







# Mpango wa Utekelezaji wa Usawa wa Austin ISD 2021

## (Hati Chanzi ya Mpango wa Kimkakati wa Wilaya)


**Ofisi ya Usawa ya AISD**

Bi. Evelin Ramos – Msaidizi-Mtendaji wa Usimamizi
Bw. Shane Whalley – Aliyekuwa Mratibu wa Usawa wa Jamii na Ujumuishaji
Bi. Sundal Ali – Mratibu wa Jamii na Ujumuishaji
Bw. Farid Razavi – Mratibu wa Usawa wa Chuo na Ujumuishaji
Dk. Tamey Williams-Hill – Mtaalamu wa Usawa na Ujumuishaji
Dk. Joseph Allen – Mkurugenzi wa Usawa, Uongozi na Mipango
Dk. Stephanie Hawley – Afisa wa Usawa

# Jedwali la Yaliyomo


Pitio la Mpango wa Utekelezaji wa Usawa (EAP) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

Wachangiaji Katika Ofisi ya Utume wa Usawa, Mfumo wa Usawa, na EAP . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .5

**Changamoto, Mapendekezo, na Itikio la Wilaya**

Hali Njema ya Mwanafunzi na Ufanisi wa Kielimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

Hali Njema ya Mwalimu na Mwajiriwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9

Utamaduni wa Huduma kwa Wateja na Heshima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 10

Usimamizi wa Kifedha na Utangulizaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 11

Marejeo Yaliyoteuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 12

**Kwa uchunguzi wa kina**

# Pitio la Mpango wa Utekelezaji wa Usawa (EAP)

## Asante

Asante kwa kushiriki katika mchakato wa Mpango wa Utekelezaji wa Usawa ili kusaidia wilaya kujifunza tunachofanya vema na mahali ambapo changamoto za usawa zinaendelea kuwapo.

Mpango huu umedhamiriwa kuandaa njia ya sauti/mahangaiko/maoni yenu kuhusishwa katika utokezaji wa mpango wa kimkakati wa wilaya nzima.




## Watu na Mchakato

Katika kipindi cha mwaka (2019–20), Ofisi ya Usawa ya AISD (OE) ilikutana nawe kwa ajili ya mfululizo wa vikao vya ukusanyaji wa habari. Lengo letu kuhusiana na vikao hivi lilikuwa kusikia mahangaiko yako, ulichofikiria kuhusu usawa katika utendaji wetu, na kutafuta maeneo ambapo tungeweza kubadilikana ili kuwa wenye usawa zaidi.




Mifano ya maoni hayo yanatia ndani

*""Kuna mambo mengi ya ajabu yanayotendeka unapokuwa na walimu wanaofanana na wewe."*

*"Nyakati fulani tunahitaji tu kupunguza mwendo na kuwasikiliza wanafunzi."*

*"Mtaala katika viwango vyote una marejeo kadhaa yanayoegemea upande mmoja na yenye ubaguzi wa rangi na kutojumuishwa kwa Asili, Afrika, Asia, na Hispania na historia ya Mashariki ya Kati."*



Zaidi ya 1,500 kati yenu kutoka katika vikundi mbalimbali walijiunga nasi, kutia ndani:

1. wanafunzi
2. watoaji huduma
3. washiriki wa jamii
4. watu binafsi/vikundi vinavyowakilisha idadi ya watu waliotengwa kihistoria
5. waelimishaji
6. mashirika ya kiraia
7. vikundi vya ushauri
8. washirika wa ndani na nje
9. vikundi vya utetezi



Wafanyakazi wa OE walisikiliza majibu yako, wakayachunguza, na kutengeneza orodha ya mapendekezo ya jamii kwa viongozi wa wilaya.







## Kutumia Hati Hii

Hati hii inaandaa habari tatu muhimu: mienendo uliyotambulisha kuwa isiyokuwa na usawa, mapendekezo yako ya suluhisho kuelekea ukosefu huo wa usawa, na hatua viongozi wa wilaya wanachukua ili kuitikia. Habari hii inawasilishwa kupitia mfuatano wa jedwali na kulingana na mambo manne yanayotangulizwa na bodi ya wadhamini (hali njema ya wanafunzi na mafanikio, hali njema ya mwalimu na mwajiriwa, utamaduni wa heshima/huduma kwa wateja, na usimamizi wa fedha na utangulizaji). Hii ni hati iliyo hai, na itasasishwa kwa ukawaida kadiri unavyoshiriki maeneo mapya ya mahangaiko na mapendekezo mapya, na kadiri AISD inavyotanguliza matokeo ya usawa kwa ajili ya wanafunzi wetu.

## Ufafanuzi wa Austin ISD wa Usawa wa Kielimu

Usawa wa kielimu unamaanisha kwamba watoto wote wanapata wanachohitaji ili kufikia ukuzi kamili kulingana na uwezo wao katika elimu na jamii.

- Kuhakikisha matokeo sawa ya juu kwa wote katika mifumo yetu ya elimu; kuondoa uwezo wa kutabiri mafanikio au kuanguka ambao kwa sasa unahusiana na vipengee vyovyote vya jamii au utamaduni;
- Kutatiza [Kukatiza] mienendo isiyokuwa na usawa, kuchunguza maegemeo yetu, na kuunda mazingira ya shule yanayojumuisha yenye tamaduni nyingi kwa ajili ya watu wazima na watoto; na
- Kugundua na kukuza zawadi za kipekee, talanta na mapendezi ambayo kila mwanadamu anayo.

## Ni nini Wanafunzi Wote Wanahitaji ili Kufanikiwa

- Walimu na wafanyikazi waliobobea kitamaduni na wenye uzoefu
- Ugunduzi na ukuzi wa zawadi, talanta na mapendezi
- Matazamio makubwa na utegemezo ili kufikia matazamio hayo makubwa
- Mahusiano mazuri na walimu na marika
- Hisi ya kuthaminiwa, upaji wa uwezo, uhusiano na usalama wa utambulisho
- Mtaala mkali, unaofaana na hali na unaojumuisha unaolenga lugha yao, utambulisho wa watu na utamaduni
- Majengo yanayotunzwa vizuri yanayotegemeza maagizo ya kisasa na yanayotegemeza utambulisho wa kitamaduni na usalama

# Wachangiaji Katika Ofisi ya Utume wa Usawa, Mfumo wa Usawa, na EAP

## Washiriki wa Jamii, Mashirika & Vikundi vya Ushauri

- Kamati ya Ushauri ya Wilaya
- Kikosi cha Kazi cha LBJ-LASA UIL
- Kikundi cha Ushirika cha LGBTQIA
- Kamati ya Ushauri ya Elimu ya Lugha Nyingi
- Wazazi & watoa huduma
- Kamati ya Ushauri ya Elimu ya Kipekee
- Kwa Ukaribu

## Washiriki wa Jamii, Mashirika & Familia

- Baraza la Timu ya Watendakazi wa PTA ya Austin
- Sauti za Elimu & Vijana za Austin
- PTA ya Blanton
- Ofisi ya Usawa ya Jiji la Austin
- Muungano kwa Ajili ya Elimu Bora wa Mashariki ya Austin
- Nenda! Austin/Vamos! Austin
- Taasisi ya Utafiti wa Sera za Miji na Jopo la Uchambuzi
- Kundi la Usawa la Maplewood
- Viongozi & wanaharakati wa shirika
- VELA
- Chama cha Ujirani wa Bustani ya Windsor

## Wanafunzi

- Shule za upili za Austin na LASA; Ukumbusho wa Upande wa Mashariki, Chuo cha mapema cha shule ya upili ya LBJ na Navarro
- Mkutano wa kushirikisha wanafunzi wa DCCE
- Majadiliano ya jopo la SOAR

## Wasimamizi & Idara/Wafanyikazi

- Wakuu wasaidizi
- Timu Tendaji ya Uongozi
- Baraza
- Wafanyikazi wa Ofisi Kuu
- Mifumo ya Mafunzo ya Mtoto
- Walezi
- Idara ya Mawasiliano & Ushirikishaji
- Mkutano wa Kilele wa Kutoa Msaada wa Elimu, Uvumbuzi & Utafiti
- Walimu wa shule za msingi, kati & upili
- Vipindi vya mazoezi ya wasimamizi wa msimu wa kuanguka
- Wasimamizi wa shule za upili
- Wafanyikazi wa Elimu ya Lugha Nyingi
- Polisi/SRO
- Wakuu
- Baraza la Usawa wa Rangi
- Timu ya Msimamizi/Timu ya Mabadiliko ya Shule
- Timu ya Ubunifu wa Teknolojia
- Watafsiri









* Vikundi vya wachangiaji na nambari zilizooredheshwa hapa ni za karibuni zaidi kufikia Januari 2021, na hazionyeshi michango baada ya tarehe hii.

# Hali Njema ya Mwanafunzi na Ufanisi wa Kielimu

| Ukosefu wa Usawa Uliotambuliwa na Washikadau | Mapendekezo ya Jamii Iliyoelimika | Hatua za Wilaya/Itikio |
|---|---|---|
| • Matokeo ya ubaguzi wa rangi katika data ya nidhamu (kimsingi kwa wanafunzi Weusi na Walatino)<br>• Mazoea ya kutengeneza sera yasiyo na usawa, yanayoegemea upande mmoja (Polisi wa AISD) | • Pitia kanuni za maadili ya mwanafunzi, na uchanganuzi wa mazoea ya nidhamu<br>• Andaa ukuzi wa kitaaluma (PD) kwa ajili ya Polisi wa AISD kuhusu ubaguzi wa rangi katika nidhamu | • Kuondoa tofauti za Rangi katika Nidhamu & Adhabu katika AISD: Mfululizo wa Mafungo ya Jamii (Ofisi ya Usawa [OE], Ofisi ya Uongozi wa Shule [OSL], Ofisi ya Mtaji wa Binadamu [HC], Mifumo ya utegemezo yenye ngazi nyingi [MTSS], Utegemezo wa Elimu ya kijamii -Kihisia /Ustadi wa Kitamaduni na Ujumuishaji [SEL/CP&I], Huduma za Utegemezaji za Wanafunzi [SSS])+<br>• Kanuni za Mwenendo wa Wanafunzi Zilizorekebishwa za mwaka wa shule wa 2021-22 (SSS)+<br>• Muda uliorekebishwa wa Vipindi vya Nidhamu vya 2021-22 (SSS)+<br>• Polisi wa AISD hupokea mazoezi katika kupunguza makali ya hali tata, tamaduni mbalimbali, afya ya akili na kushughulikia hali ya dharura (AISD PD)+ |
| • Usimamizi wa vituo usio na usawa katika shule zilizo katika jamii zilizotengwa<br>• Majina ya shule na vitambulisho visivyozingatia tamaduni/vyenye ubaguzi kuhusiana na Wamarekani wa Asili na wanafunzi na jamii za asili | • Simamia vituo kwa kutumia sera na mazoea ya usawa<br>• Amuru uwepo wa PD katika ustadi wa tamaduni katika idara ya Operesheni<br>• Shirikisha jamii katika majadilianao kuhusu majina/nembo zinazohusianishwa na shule /vitambulisho vyote | • Itifaki ya mipango ya vifaa vya muda mrefu inayolenga usawa (Operesheni)*<br>• Kupanga kwa ajili ya uchanganuzi wa wilaya nzima wa usawa wa mshiriki wa tatu (OE)*<br>• Wilaya itaendelea kuhusisha jamii za shule kuhusiana na kutafutia shule majina (Idara ya Mawasiliano na Ushirikishaji [DCCE])+ |
| • Uwajibikaji mchache kuelekea usawa katika wilaya nzima | • Tokeza hatua za uwajibikaji zinazolenga usawa katika wilaya nzima zinazozidi vipimo vilivyopo | • Ipe umuhimu mikakati ya Mipango ya Hatua za Usawa katika utokezaji wa Mpango wa Kimkakati wa wilaya (Timu ya Uongozi wa Utendaji [ELT])* |

* = Vitendo ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sasa/hatua ya kupanga
+ = Vitendo ambavyo vimeanza na vinasubiri matokeo
† = Vitu vya kuchukuliwa hatua na matokeo yaliyoandikwa

# Hali Njema ya Mwanafunzi na Ufanisi wa Kielimu

| Ukosefu wa Usawa Uliotambuliwa na Washikadau | Mapendekezo ya Jamii Iliyoelimika | Hatua za Wilaya/Itikio |
| --- | --- | --- |
| • Uhitaji wa maendeleo ya uongozi kwa ajili ya usawa wa rangi na ujumuishaji | • Amuru uwepo wa PD inayoendelea kuhusisha na inayopinga ubaguzi wa rangi katika uongozi wote wa wilaya | • Utokezaji wa ueneaji na mpangilio wa ustadi wa kitamaduni upatikanao wa wilaya nzima / Kupinga-ubaguzi wa rangi katika PD kwa waajiriwa wote (OE, HC, SEL/CP&I)*<br>• Wakuu wataendelea kupokea mazoezi katika itikio la kitamaduni (OSL)+<br>• Bodi ya Wadhamini ya AISD na ELT itashiriki katika ustadi wa kitamaduni katika mwezi wa Agosti 2021 (OE)* |
| • Ukusanyaji uliodhibitiwa na matumizi yanayofaa ya data iliyogawanywa katika michakato ya kufanya maamuzi | • Tathmini upya mbinu za kukusanya data na ukuze matumizi ya data iliyogawanywa katika michakato ya kufanya maamuzi | • Maombi yote ya data ni pamoja na data iliyogawanywa katika vikundi vidogo vidogo (HC)*<br>• Maamuzi yanafanywa kwa kuchanganua data iliyogawanywa katika vikundi vidogo vidogo (ELT)+ |
| • Vizuizi kwa usawa katika kufikia programu kali za elimu zenye ubora wa juu (vizuizi katika mchakato wa kutuma maombi kwa programu za kitaaluma/sumaku, vizuizi vinavyotegemea lugha, na vizuizi vinavyotegemea rangi/asili) | • Tokeza mpango wa wilaya nzima ili kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika programu zote, ukizingatia idadi ya wanafunzi waliotengwa<br>• Tambua matokeo ambayo idadi ya walioandikishwa imekuwa nayo kuelekea ufungaji wa shule<br>• Unda idara/ofisi inayowajibika kuelekea uandikishaji na ushirikishaji<br>• Fanya ukaguzi rasmi wa usawa wa mshiriki wa tatu | • Uchanganuzi wa mchakato wa sasa wa kutuma maombi kwa program maalum/program sumaku za shule (pamoja na maoni kutoka kwa jamii) (OSL, OE)+<br>• Kupanga kwa ajili ya uchanganuzi wa usawa wa mshiriki wa tatu (OE)*<br>• Wilaya itaajiri Mkurugenzi Mtendaji wa Uandikishajina Utetezi (Mkuu wa Wafanyakazi)+ |

* = Vitendo ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sasa/hatua ya kupanga
\+ = Vitendo ambavyo vimeanza na vinasubiri matokeo
† = Vitu vya kuchukuliwa hatua na matokeo yaliyoandikwa

# Hali Njema ya Mwanafunzi na Ufanisi wa Kielimu

| Ukosefu wa Usawa Uliotambuliwa na Washikadau | Mapendekezo ya Jamii Iliyoelimika | Hatua za Wilaya/Itikio |
|---|---|---|
| • Upungufu wa fursa kwa uwakilishi wa wanafunzi (kujitetea wenyewe) na sauti ya mwanafunzi katika michakato ya kufanya maamuzi<br>• Utegemezo uliodhibitiwa kwa wanafunzi kwa kutegemea utambulisho wao: rangi/asili, mwelekeo wa kijinsia/utambulisho wa jinsia, lugha kuu, namba ya ZIP, na uwezo<br>• Utegemezo wa elimu ya kijamii-kihisia isiyopatana (SEL) kwa wanafunzi | • Andaa PD inayolenga usawa kwa ajili ya Ofisi ya Uongozi wa Shule, Masomo, SEL, Huduma za Wanafunzi<br>• Fanya ukaguzi rasmi wa usawa wa mshiriki wa tatu | • Utokezaji wa ueneaji na mpangilio wa Ustadi wa Kitamaduni upatikanao wa wilaya nzima/Kupinga Ubaguzi wa Rangi PD kwa waajiriwa wote (OE, HC, SEL/CP&I)*<br>• Kupanga uchanganuzi wa usawa wa wilaya nzima wa mshiriki wa tatu (OE)*<br>• Uongozi wa Shule umewaandalia walimu wakuu maendeleo ya kitaalamu kuhusiana na Kubuni Uwezo wa Kushughulika na Tamaduni Mbalimbali (OSL)+<br>• Bodi ya Wadhamini na ELT zitahudhuria maendeleo ya kitaalamu mwezi wa Agosti 2021 (OE)*<br>• Katika mwaka wa 2021-22, Msimamizi atabuni Bodi ya Matineja (Msimamizi)* |
| • Uhitaji wa walimu na wafanyikazi tofauti zaidi/wataalamu ili kutegemeza vikundi vya wanafunzi waliotengwa | • Ajiri na uhifadhi wafanyikazi tofauti wenye ustadi wa kitamaduni | • Uchanganuzi wa mazoea ya kuajiri ya wilaya (HC)*<br>• PD kwa ajili ya Ofisi ya Mtaji wa Binadamu kuhusiana na mazoea ya usawa katika kuajiri (OE)* |
| • Elimu ya kitaaluma isiyopatana ili kutegemeza mazoea yanayokubalika kitamaduni/endelevu kwa ajili ya walimu na wafanyikazi | • Tekeleza mpango wa PD wa wilaya nzima unaolenga usawa wa rangi, ustadi wa kitamaduni na ujumuishaji, ufundishaji unaokubalika kitamaduni/endelevu, na mazoea ya elimu ya kupinga ubaguzi wa rangi | • Utokezaji wa ueneaji na mpangilio wa Ustadi wa Kitamuduni upatikanao wa wilaya nzima / Kupinga Ubaguzi wa Rangi kwa waajiriwa wote (OE, HC, SEL/CP&I)* |
| • Ukosefu wa mtaala unaokubalika kitamaduni/endelevu<br>• Vitu vichache vya kuchagua katika mtaala mbadala (k.v. programu za biashara)<br>• Mahangaiko kuhusiana na mbinu ya kufundisha ili kujaribu ikilinganishwa na umahiri wa yaliyomo | • Tekeleza mikakati ya, utokezaji wa mtaala unaokubalika kitamaduni/endelevu, unaopinga ubaguzi wa rangi<br>• Tokeza uwezo kati ya Wasomi ili kushirikisha na kupata maoni kutoka kwa jamii zilizotengwa katika mchakato wa kutokeza mtaala | |

* = Vitendo ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sasa/hatua ya kupanga
+ = Vitendo ambavyo vimeanza na vinasubiri matokeo
† = Vitu vya kuchukuliwa hatua na matokeo yaliyoandikwa

# Hali Njema ya Mwalimu & Mwajiriwa

| Ukosefu wa Usawa Uliotambuliwa na Washikadau | Mapendekezo ya Jamii Iliyoelimika | Hatua ya Wilaya/Itikio |
|---|---|---|
| • Fursa chache za kuwakilisha walimu (kujitetea wenyewe) na sauti ya mwalimu katika michakato ya kufanya maamuzi | • Boresha na uendeleze utamaduni na mazingira ya kazi yanayojumuisha kwa waajiriwa ukizingatia kihususa wale walio na utambulisho uliotengwa<br>• Changanua na upitie mifumo iliyopo ya utegemezo inayoandaa nafasi salama kwa wafanyikazi wa wilaya kueleza maoni yao.<br>• Tokeza na utegemeze njia zitakazowawezesha wasimamizi wa chuo kushiriki katika maafikiano/mawasiliano na wafanyikazi | • Katika mwaka wa shule wa 2020-21, Msimamizi alifanya Mikutano ya kila mwezi ya Walimu Kujadiliana na Vikundi Vinavyolenga Walimu Wakuu. Hili litaendelea katika mwaka wa shule wa 2021-22 (Msimamizi)+<br>• Katika mwaka wa shule wa 2021-22, Wakurugenzi Watendaji wa kila kiwango cha shule watafanya mikutano ya kila mwezi ya vikundi vinavyolenga walimu (OSL)* |
| • Ukosefu wa usawa katika kuajiri na mbinu za kupeana marupurupu<br>• Mazoea ya kuajiri yasiyo na usawa na yasiyojumuisha na yasiyohusisha maoni ya jamii | • Ongeza kuajiri na kuhifadhi walimu/ wafanyikazi walio na utambulisho uliotengwa<br>• Waandalie viongozi wa uajiri na PD ili kutegemeza mazoea ya usawa katika kuajiri<br>• Changanua na upitie itifaki za kamati za chuo za mahojiano ya kuajiri | • Idara ya Kushughulikia Waajiriwa imebadilisha mazoea ya kuleta waajiriwa wapya (HC)+<br>• Idara ya Kushughulikia Waajiriwa inabuni vikundi vya kijamii vya waajiriwa wenye tamaduni zinazofanana (HC)*<br>• Idara ya Kushughulikia Waajiriwa ina mtu hususa aliye na wajibu wa kuendeleza maendeleo ya walimu na wasimamizi kutoka HBCUs na HSIs (HC)+<br>• Maswali ya mahojiano yamerekebishwa (HC)+<br>• Viwango vya utathmini vimerekebishwa (HC)+ |
| • Maendeleo ya kitaaluma yasiyopatana (PD) yanayopendekeza na kutegemeza mazoea ya usawa | • Tokeza PD ya wilaya nzima inayozingatia usawa wa rangi, ustadi wa kitamaduni na ujumuishaji, na mazoea ya kupinga ubaguzi | • Utokezaji wa ueneaji na mpangilio wa Ustadi wa Kitamaduni upatikanao wa wilaya nzima/ Kupinga Ubaguzi wa Rangi PD kwa waajiriwa wote (OE, HC, SEL/CP&I)* |

* = Vitendo ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sasa/hatua ya kupanga
+ = Vitendo ambavyo vimeanza na vinasubiri matokeo
† = Vitu vya kuchukuliwa hatua na matokeo yaliyoandikwa

# Utamaduni wa Huduma kwa Wateja na Heshima

| Ukosefu wa Usawa Uliotambuliwa na Washikadau | Mapendekezo ya Jamii Iliyoelimika | Hatua ya Wilaya/Itikio |
|---|---|---|
| • Ukosefu wa mawasiliano ya hatua za uwajibikaji wa usawa na jamii zilizotengwa | • Unda na uwasilishe hatua za uwajibikaji katika wilaya nzima zinazoangazia kuondoa ubaguzi katika upatikanaji na matokeo<br>• Tokeza itifaki ili kushiriki michakato ya kufanya maamuzi ya wilaya na washikadau katika jamii | • Kuondoa tofauti za Rangi katika Nidhamu & Adhabu katika AISD: Mfululizo wa Mafungo ya Jamii (OE, OSL, HC, MTSS, SEL/CP&I, SSS)+<br>• Majadiliano ya Jamii ya Msimamizi na Mazungumzo ya Wilaya (Msimamizi)+<br>• Kupanga kwa ajili ya uchanganuzi wa usawa wa mshiriki wa tatu katika wilaya nzima (OE)* |
| • Upatikanaji uliodhibitiwa na ushirikishaji wa moja kwa moja na watoa huduma na familia katika jamii zilizotengwa<br>• Fursa zilizopunguzwa kwa mtoa huduma/uwakilishi wa familia (kujitetea mwenyewe) na sauti ya mtoa huduma/familia katika michakato ya kufanya maamuzi ya wilaya | • Tokeza mpango wa wilaya nzima wa kuongeza ushirikishaji wa jamii, ukitilia mkazo idadi ya jamii zilizotengwa<br>• Ajiri na uhifadhi wafanyikazi wenye uwezo kitamaduni wanaoweza kusaidia washikadau katika jamii kujua kutumia mfumo wa AISD | • Uundaji wa Kamati ya Ushauri wa Usawa (Msimamizi)+ |
| • Mazoea ya mawasiliano yasiyo na uwazi na yasiyojumuisha kuhusiana na maamuzi mazito | • Wasiliana na jamii kupitia lugha zote na mbinu nyingi na kwa wakati unaofaa<br>• Tayarisha uongozi wa wilaya kuwashirikisha na kuwasikiliza washikadau katika jamii, na kufanyia kazi mahitaji yaliyotajwa ya jamii zilizotengwa | • Majadiliano ya Jamii ya Msimamizi na Mazungumzo ya Wilaya (Msimamizi)+<br>• Ili kuongeza uwazi, stakabadhi zote za ajenda ya bodi huwekwa wiki mbili mapema kabla ya bodi kuchukua hatua (Uhusiano wa Serikali na Huduma za Bodi)+ |
| • Uhitaji uliotambuliwa wa kujenga mahusiano halisi/kuaminiana na jamii zilizotengwa | • Ongeza uboreshaji wa uwezo ili uongozi wa wilaya ujifunze kukuza mahusiano ya kuaminiana na washiriki wa jamii zilizotengwa na wanafunzi | • Kuondoa Tofauti za Rangi Katika Nidhamu & Adhabu katika AISD: Mfululizo wa Mafungo ya Jamii (OE, OSL, HC, MTSS, SEL/CP&I, SSS)+<br>• Majadiliano ya Jamii ya Msimamizi na Mazungumzo ya Wilaya (Msimamizi)+<br>• Operesheni: Unganisha Upya (2021)(OSL)+ |

* = Vitendo ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sasa/hatua ya kupanga
+ = Vitendo ambavyo vimeanza na vinasubiri matokeo
† = Vitu vya kuchukuliwa hatua na matokeo yaliyoandikwa

# Usimamizi wa Kifedha & Utangulizaji

| Ukosefu wa Usawa Uliotambuliwa na Washi-kadau | Mapendekezo ya Jamii Iliyoelimika | Hatua ya Wilaya/Itikio |
|---|---|---|
| • Uangaziaji uliodhibitika katika usawa katika ugawaji wa bajeti<br>• Uangaziaji mchache katika usawa katika ugawaji wa rasilimali za jumla<br>• Ukosefu wa usawa katika utegemezaji wa kifedha wa wafanyikazi/kuajiri | • Idara za Fedha, Bajeti na Utekelezaji na Uwajibikaji wa Taifa & Shirikisho zinapaswa kutanguliza mapitio ya michakato na mifumo ambapo maamuzi ya ugawaji wa fedha kwa mitaa, taifa na shirikisho hufanywa na fedha hugawanywa<br>• Kila idara na chuo inapaswa kushirikisha Sanduku la Vifaa la Mipango Inayoangazia Usawa, Utathmini & Utengenezaji wa Bajeti: Vifaa Vya Kubuni Upya Hisia ya Mji ya Matokeo ya Usawa kwa ukawaida<br>• Kila jamii na chuo inapaswa kushirikisha washirika wa jamii zilizotengwa au kamati za wafanya-maamuzi zilizo chuoni katika mchakato wa kutengeneza bajeti<br>• Kila idara na chuo inapaswa kufanya mabadiliko yanayohitajika ya bajeti yakitegemea mahitaji na mapendezi ya wanafunzi waliotengwa<br>• Andaa maendeleo ya kitaalamu kwa wafanyikazi wa fedha, bajeti, na operesheni kuhusiana na kutengeneza bajeti inayotegemea usawa na kufanya maamuzi | • Usawa wa AISD katika Vifaa vya Kutengeneza Bajeti (mchakato wa wachukuaji wa mapema) (OE)+ |

* = Vitendo ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sasa/hatua ya kupanga
\+ = Vitendo ambavyo vimeanza na vinasubiri matokeo
† = Vitu vya kuchukuliwa hatua na matokeo yaliyoandikwa

# Marejeo Yaliyoteuliwa

Ufafanuzi wa Austin ISD wa Usawa wa Kielimu uliotolewa katika https://nationalequityproject.org/

Mfumo wa Usawa wa Austin ISD : https://www.austinisd.org/sites/default/files/dept/equity-office/docs/Equity-Framework-%26-Key-Questions.pdf

Chardin, M., & Novak, K. (2021). Usawa kwa muundo: Kuandaa kulingana na uwezo na ahadi ya UDL. Corwin.

Muungano wa Serikali katika Rangi na Usawa. (2021). Vifaa na rasilimali. https://www.racialequityalliance.org/tools-resources/

Johnson, J. (2019). Mazoea ya Ufundishaji kutoka kwa shule bora zaidi katika majiji Marekani. Routledge.

Love, B. (2019). Tunataka kufanya zaidi ya kuishi: Mafundisho ya uondoaji na ufuatiliaji wa uhuru wa kielimu. Beacon Press.

Muhammad, G. (2020). Kukuza fikra: Mfumo wa usawa kwa ajili ya itikio zuri kiujuzi kitamaduni na kihistoria. Scholastic Inc







# Mpango wa Utekelezaji wa Usawa wa Austin ISD 2021